



TANGAZO

MPANGO WA UFADHILI WA WALIMU (TSP) – PUNGUZO LA ADA YA MASOMO KWA 50%

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kipo katika mkakati wa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuongeza upatikanaji wa elimu ya juu yenye ubora wa hali ya juu kwa walimu waliopo makazini. Lengo la mpango huu wa punguzo la ada ni kuimarisha uwezo wa rasilmali watu ili kupata maarifa, ujuzi, na umahiri unaohitajika ili kusaidia mageuzi katika sekta ya elimu nchini. OUT ni Chuo kinachotoa elimu kwa njia ya masafa, huria na mtandao hivyo kinaweza kuwafikia wanafunzi wake katika maeneo yao bila kuathiri shughuli zao za kila siku za kijamii, kiuchumi na kiutumishi.

1. Vigezo vya Ufadhili

- Mnufaika lazima awe mwalimu kwa taaluma, anayefundisha katika shule ya msingi au sekondari ya umma.
- Walimu wanapaswa kuthibitishwa na kuidhinishwa na mwajiri wao kutoka katika wilaya au manispaa zao kulingana na mipango yao ya maendeleo ya wafanyakazi.
- Waombaji wanapaswa kuwa na sifa zinazohitajika za kujiunga na programu ya diploma au shahada ya kwanza wanayoichagua inayotolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Waombaji waliofanikiwa watapata punguzo la 50% ya ada ya masomo kwa mwaka wa masomo wa 2024/25 lakini watatakiwa kulipa ada zote zisizohusiana na masomo kama ada ya mtihani, usajili, mchango wa serikali ya wanafunzi (OUTSO), kadi ya utambulisho ya mwanafunzi, mahafa-

li, nakala za matokeo, n.k.

- Punguzo la 50% litahusu tu ada ya masomo kwa kozi zote ambazo mwanafunzi atasajili kwa mwaka wa masomo 2024/25 kwa programu zote zilizo chini ya ufadhili huu, yaani diploma au shahada ya kwanza.

2. Utaratibu wa Maombi

- Mwombaji wa ufadhili lazima awe amechaguliwa kwenye programu husika.
- Fomu ya maombi ya ufadhili inapatikana kwenye vituo vyote vya mikoa vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Fomu za maombi zilizojazwa lazima zipitishwe kwa mwajiri (i.e. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Mji, au Wilaya).
- Fomu zilizokamilika ziwasilishwe kwa Mkurugenzi wa Kituo cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania cha Mkoa husika.
- Watakaofanikiwa kupata ufadhili huu watajulishwa kwa barua.

3. Tarehe ya Mwisho ya Maombi ya Ufadhili kwa Mwaka wa Masomo 2024/25

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi kwa muhula wa Aprili, mwaka wa masomo **2024/25** ni tarehe **31 Machi 2025**.

4. Kwa Maelezo Zaidi

Tafadhali tembelea ofisi za vituo vya mikoa vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania au wasiliana na mratibu kwa namba hii: **0762 800 142**.

Imetolewa na: Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti & Ushauri wa Kitaalamu)